Kanuni za Utoaji

Leseni kwa

Makao ya Kulea yaliyoko Vermon

VERMONT

IDARA YA WATOTO NA FAMILIA

KITENGO CHA HUDUMA KWA FAMILIA

Taarifa kwa Wasomaji

Kanuni hizi zilianza kutumika mnamo Septemba mwaka 1992 na zinaonyesha sheria ya jimbo iliyokuwa ikitumika wakati huo. Visanduku vyilivyowekewa kivuli vinaelezea mahitaji ya kisheria yaliyoongezwa baada ya kupitishwa kwa kanuni hizi na taarifa nyingine zinazobainisha zaidi.

Kwa Taarifa Zaidi

Leseni ya Makazi na Kitengo Maalum cha Uchunguzi
Kitengo cha Huduma kwa Familia
Idara ya Watoto na Familia Vermont
(802) 241-2131

dcf.vermont.gov/fsd

YALIYOMO

MADHUMUNI YA KANUNI 4
MAMLAKA KISHERIA 4
Utoaji Leseni kwa Huduma ya Kulea na Kuwekwa Makazi (33 VSA, 3501) 5
Vifungu vya Utawala (33 VSA, 306) 5
TARATIBU 6
Utoaji, Utoaji upya, na Masharti 6
Mbadala wa kanuni 7
Kukataa, Kufuta, na Kusimamisha 7
Haki za kukata Rufaa 8
Kumbukumbu za Makao ya Kulea 9
Masharti ya Leseni 9
MAOMBI NA TATHMINI YA LESENI 10
SIFA ZA WAZAZI WA KULEA 11
MAJUKUMU YA WAZAZI WALEZI 12
Utunzaji na Usimamizi wa Watoto wa Kulea 12
Mazingira ya Nyumba, Jamii, na Shughuli za Familia 13
Usiri na Faragha 14
Mahusiano na Familia ya Mtoto 14
Nidhamu 14
Matunzo Kiafya 16
Chakula na Lishe 16
Dini na Urithi Kiutamaduni 17
Kutoa Taarifa na Tahadhari 17
MAZINGIRA YA NJE 18
Usalama na Matengenezo ya Jumla 18
Usalama kwa Moto 19
Vyumba vya kulala 21
Usafirishaji 23
FASILI 25

MADHUMUNI YA KANUNI

010 Chini ya Mamlaka ya 33 VSA, 3501, Idara ya Watoto na Familia inahusika katika kutoa leseni kwa makao ya kulea watoto.

Kanuni hizi zimeanzishwa ili kuhakikisha matunzo na usalama wa watoto ambao wanahitaji kuishi katika makao mengine ambayo si yao. Leseni hutolewa ikiwa makao ya kulea na anayetarajiwa kuwa mlezi(walezi) atatimiza kanuni hizi.

Idara ikigundua kwamba mwombaji(waombaji) au mmiliki(wamiliki) leseni hawataki au hawawezi kutimiza kanuni hizi, leseni haitatolewa au itabatilishwa.

Kanuni muhimu za kuhakikisha ustawi wa mtoto kuhusu mambo yafuatayo:

1. Usalama na utoshaji wa nyumba kwa ajili ya utunzaji watoto;
2. Sifa binafsi na mahusiano ya kijamii ya mlezi (walezi) na wanafamilia wengine katika kaya;
3. Kujitoa kwa malezi ya watoto, na uwezo na utayari wa familia ya kulea kufanya kazi kwa kushirikiana ili kupata mpango wa kulea wa mtoto; na
4. Uwezo wa familia walezi kutoa uzoefu chanya, na wenye kujenga kwa watoto wote wanaowatunza.

MAMLAKA KISHERIA

020 Sheria ya Vermont inayosimamia utoaji wa leseni ya vituo vya utunzaji watoto imewekwa katika Kifungu namba 33 cha Sheria za Vermont Vilivyoelezwa kama ifuatavyo:

Utoaji Leseni kwa Huduma ya Kulea na Kuwekwa Makazi (33 VSA, 3501)

a. Mtu, yeyote mwingine isipokuwa mfanyakazi wa idara ndani ya shirika la huduma kwa wanadamu, hatamuweka mtoto yeyote katika malezi kwa zaidi ya siku 15 mfululizo isipokuwa kama mtu huyo ana leseni kutoka kwenye idara ya kufanya hivyo au ni mfanyakazi wa shirika la kuwaweka watoto mwenye leseni ya idara hiyo.

b. Mtu hatapokea, kumsitiri, au kukaa na mtoto yeyote katika malezi ya watoto kwa siku zaidi ya 15 mfululizo isipokuwa kama ana leseni kutoka kwenye idara ya kufanya hivyo. Kifungu hiki hakitatumika kwa makao ya kulea yaliyoidhinishwa na idara ndani ya shirika la huduma kwa wanadamu au na shirika la kuwaweka watoto lenye leseni wala hakitatumika kwa vituo ambavyo mafunzo ya elimu au kiufundi ni huduma ya msingi na malezi ni huduma ya kusaidia tu.

c. Sehemu hii haitazuia haki ya mahakama, mzazi, mlezi, au ndugu kumweka mtoto, wala haki ya mtu ambaye hafanyi biashara ya kutoa malezi au malezi ya mtoto kupokea, kumsitiri, na kukaa na mtoto ambapo tafakuri haihitajiki au kupokelewa kwa ajili ya matunzo ya mtoto.

Vifungu vya Utawala (33 VSA, 306)

Kifungu hiki kitatumika kwa leseni zote na maombi ya leseni, ambayo kamishna au idara inaweza kutoa, isipokuwa ikiwa kwa mahsusi imesemwa vinginevyo.

1. Kamishna atatoa kanuni zinazoongoza maombi ya, na utoaji, ubatilishaji, muda na utoaji upya wa leseni na usajili. Katika kanuni anaweza kuagiza viwango na masharti yanayotakiwa kutimizwa, kumbukumbu za kutunza, na ripoti zinazotakiwa kuwasilishwa. Leseni na usajili vitakuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia siku ilipotolewa isipokuwa ikiamriwa tofauti na kanuni.
2. Majengo yenye leseni au usajili yanaweza kutembelewa na kukaguliwa na idara kwa saa zinazofaa. Mtu anayepokea leseni au usajili ataruhusu kutembelewa na ukaguzi, na uchunguzi wa kumbukumbu anazotakiwa kuwa nazo.
3. Leseni au usajili unaweza kubatilishwa kwa sababu baada ya kusikilizwa na inaweza kusimamishwa katika hali zinazohatarisha afya haraka, usalama, au ustawi wa watu wanaotunzwa wa mwenye leseni au aliyesajiliwa.
4. Kabla ya leseni kutolewa, idara itatembelea na kukagua majengo ambayo leseni hiyo imeombwa kwayo, na kufanya uchunguzi zaidi.

TARATIBU

Utoaji, Utoaji upya, na Masharti

030 Leseni ya awali itakuwa halali kwa mwaka mmoja isipokuwa kama imeamriwa vinginevyo na kamishna, isipokuwa wakati leseni imebatilishwa au kufutwa kisheria.

031 Utoaji upya wa leseni utafanyika kila mwaka isipokuwa kama ikiagizwa vinginevyo na kamishna. Wakati makazi yanakaguliwa kwa ajili ya kupewa tena leseni, mamlaka ya leseni ya jimbo yatapitia ufuatwaji wa kanuni hizi na

itatathmini ni vyema kiasi gani mahitaji ya watoto wanaotunzwa na mzazi(wazazi) yametimizwa.

032 Leseni ni halali tu kwa mtu(watu) waliotajwa kwenye leseni na kwa majengo yaliyopewa leseni hiyo.

033 Idara inaweza kuweka masharti kwenye leseni, ikiwa ni pamoja na sharti la kutoa matunzo kwa mtoto maalum tu.

034 Mamlaka ya utoaji leseni ya jimbo inaweza kumtaka mtu yeyote kwenye kaya au mtu yeyote anayetunza au kuwaangalia watoto wa kulea kila mara, haijalishi kama yeye ni mwombaji au mwenye leseni, awasilishe wadhamini na kutoa taarifa nyingine kadri mamlaka ya leseni ya jimbo itakavyoona inafaa.

Mbadala wa kanuni

035 Mamlaka ya leseni ya serikali inaweza kutoa mbadala kwa kanuni maalum ikitambua kwamba mwombaji au mwenye leseni atatimiza lengo la kanuni hiyo. Mbadala wa kanuni unaweza kuwa na masharti na mipaka.

036 Mbadala wa kanuni ni halali kwa muda wote wa leseni, isipokuwa ikifutwa au kuzuiliwa na mamlaka ya leseni ya jimbo, na inaweza kuhuishwa.

Kukataa, Kufuta, na Kusimamisha

037 Leseni inaweza kukataliwa au kufutwa ikiwa mwombaji au mwenye leseni atashindwa kutimiza kanuni zozote za utoaji leseni.

038 Leseni inaweza kukataliwa au kufutwa ikiwa mwombaji, mwenye leseni au mwanafamilia mwingine katika kaya:

038.1 Ameshtakiwa au kuhukumiwa kwa kosa la jinai;

038.2 Ana shida kwa sasa, ambazo hazijasuluhishwa za unywaji wa pombe au kemikali nyingine; au

038.3 Amemnyanyasa au kumtelekeza mtoto.

039 Leseni inaweza kusimamishwa ikiwa kuna, hali katika makao ya kulea, inayohatarisha moja kwa moja afya, usalama, au ustawi wa watu wanaotunzwa na mwenye leseni.

040 Leseni inaweza kukataliwa, kubatilishwa, au kuwekewa mipaka ikiwa kuna hali tata isiyo ya kawaida katika makao ya kulea, ambayo inaathiri utunzaji unaofaa wa watoto. Hali hizo ni pamoja na, bali sio tu talaka, kutengana, kifo, ukosefu wa ajira, ugonjwa mbaya au kuumia, au ujio wa mwanafamilia mgeni kwenye kaya.

041 Leseni inapokataliwa, kusimamishwa, au kufutwa, taarifa kwa maandishi inayoonyesha sababu za kukataa au kufutwa itapelekwa kwa mwombaji(waombaji) au mwenye(wenye) leseni.

Haki za kukata Rufaa

042 Pale ambapo idara inapendekeza kufutwa kwa leseni ya makao ya kulea, mwenye leseni atapewa fursa ya kusikilizwa na kamishna au msimamizi wa kamishna kabla ya tarehe ya kufutwa kuanza.

043 Mwenye leseni au mwombaji wa leseni ambaye hakubaliani na uamuzi wa kitengo cha utoaji leseni atasikilizwa kwa haki mbele ya Bodi ya Huduma kwa Wanadamu akiomba asikilizwe ndani ya siku 30 tangu idara itoe uamuzi.

Kumbukumbu za Makao ya Kulea

044 Idara itaweka kumbukumbu ya kila mwombaji na mwenye leseni ya makao ya kulea. Kumbukumbu zitajumuisha maombi, barua za wadhamini, orodha za kukagulia ufuataji kanuni, ripoti za leseni na madokezo kuhusu mawasiliano na au kuhusu mwombaji(waombaji) au mwenye(wenye) leseni. Kumbukumbu hizi ni mali ya idara na zitatolewa tu kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

045 Idara, kwa kuombwa, itampa mwombaji (waombaji) au mwenye(wenye) leseni husika taarifa zote zilizomo kwenye kumbukumbu ya leseni isipokuwa taarifa iliyopokelewa kutoka kwa watu wasiohusika moja kwa moja, kama barua za wadhamini na taarifa ya siri kulingana na sheria. Idara, baada ya kupokea taarifa iliyoandikwa kutoka kwa mwombaji(waombaji) au mwenye(wenye) leseni husika, itawapatia watu wasiohusika moja kwa moja taarifa zote zilizomo kwenye kumbukumbu ya leseni ya mwombaji au mwenye leseni ambayo angeweza kufikia.

Masharti ya Leseni

046 Idadi kamili ya watoto wanaoishi au wanaotunzwa mara kwa mara katika makao ya kulea itaamuliwa na tathmini ya uwezo wa familia wa kutoa matunzo na usimamizi unaofaa na kwa kiwango cha nafasi ya sehemu ya kuishi kwenye makao hayo.

047 Idadi ya watoto wanaolelewa walio katika makao ya kulea yenye leseni haitazidi nne.

048 Idadi ya watoto wa kulea ambao makao ya kulea yana leseni ya awali haizidi mbili kwa muda wa leseni ya kwanza.

049 Familia ya kulea hairuhusiwi kutunza watoto zaidi ya wanne wenye umri wa chini ya miaka sita wakati wowote ule, ikiwa ni pamoja na watoto wanaoishi kwenye nyumba hiyo na

watoto wanaotunzwa kwa muda.

050 Hakutakuwa na watoto zaidi ya wawili wenye umri wa chini ya miezi 24 wanaoishi au kutunzwa mara kwa mara katika makao ya kulea.

051 Jumla ya watoto wanaoishi katika makao ya kulea haitazidi sita.

MAOMBI NA TATHMINI YA LESENI

101 Mtu au wenzi wanaoomba leseni watawasilisha maombi kwa maandishi kwa kutumia fomu iliyotolewa na mamlaka ya leseni ya jimbo.

102 Wanandoa wanaoishi pamoja lazima watume maombi kwa pamoja.

103 Waombaji na wenye leseni wata:

103.1 Toa taarifa kamili na ya ukweli kuhusu maombi ya leseni na katika mchakato wa utoaji leseni.

103.2 Shirikiana kikamilifu na mtoa(watoa) leseni katika kuamua ikiwa kanuni zote za leseni zimetekelezwa na zinaendelea kutekelezwa.

103.3 Shirikiana kikamilifu na uchunguzi wowote wa leseni.

104 Maombi mapya yanaweza kuhitajika ikiwa:

104.1 Maombi ya leseni yaliondolewa na waombaji wanawasilisha tena maombi;

104.2 Idara iliwanyima, ilifuta, au ilikataa kuhuisha leseni ya makao na wale waliokataliwa, waliobatilishiwa, au walionyimwa wanataka kurejeshwa kuwa makao ya

kulea;

104.3 Nyumba ilikuwa na leseni na mwenye leseni aliomba kufunga makao kwa hiari;

104.4 Leseni imekuwa batili kwa sababu ya kuhamia kituo tofauti; au

104.5 Mabadiliko yanayoathiri kustahiki kwa leseni yametokea.

SIFA ZA WAZAZI WA KULEA

200 Wanakaya walio katika makao ya kulea lazima wawe wawajibikaji, thabiti kihisia, wakomavu kihisia wenye tabia nzuri kama ilivyoonyeshwa na utendaji wa zamani na sifa ya jumla.

201 Waombaji na wenye leseni wataonyesha:

201.1 Mwelekeo mzuri wa mahusiano ya kijamii na baina ya watu;

201.2 Maarifa juu ya ukuaji wa mtoto na mahitaji ya watoto;

201.3 Uwezo wa kuadhibu kwa njia inayostahili na yenye mafunzo;

201.4 Matarajio halisia kuhusu tabia ya watoto wa kulea;

201.5 Tafakuri nzuri ya kuamua;

201.6 Uhuru uliopo wa kutotumia dawa za kulevya, na kusuluhisha vyema utumiaji mbaya wa zamani wa pombe au mihadarati;

201.7 Utunzaji wa uwajibikaji na/au kupanga kwa ajili ya watoto wao, ikiwemo watoto wasiotunzwa na mwombaji au mwenye leseni;

201.8 Marekebisho thabiti ya kihisia baada ya mabadiliko

yoyote makubwa katika uhusiano wa karibu baina ya watu au hali nyingine za maisha.

202 Kila mtu mzima anayemtunza mtoto nyumbani ataonyesha uwezo wa kuwa yeye ni mfano bora kwa watoto.

203 Wanakaya wote watakuwa hawana matatizo ya hali za kimwili, upungufu wa kiakili, au shida za kihisia, ambazo zinaweza kuwa na athari mbaya kwa ustawi wa mwili au wa kihisia wa watoto wa kulea.

204 Walezi wa msingi wanapaswa kuwa na umri wa angalau miaka 21.

205 Wazazi wa kulea wataonyesha kwamba wana kipato cha kutosha kuitunza familia, hata bila ya watoto wa kulea, bila kutegemea malipo ya msingi ya malezi.

MAJUKUMU YA WAZAZI WALEZI

300 Wazazi wa kulea watashiriki katika mafunzo yaliyopangwa na shirika la kuwaweka watoto ili yawe muhimu kwa utunzaji wa watoto wa kulea.

Utunzaji na Usimamizi wa Watoto wa Kulea

301 Wazazi wa kulea watimize mahitaji ya kimwili, kihisia, ukuaji na ya kielimu ya kila mtoto wa kulea, kulingana na mpango wa kulea wa mtoto anayetunzwa.

302 Wazazi wa kulea watatoa au kupanga usimamizi unaofaa kwa kila umri wa mtoto na kiwango cha ukuaji.

303 Wazazi wa kulea watakuwa na mpango wa kutoa huduma mbadala inayofaa wasipokuwepo kwa sababu za kikazi au madhumuni mengine.

304 Mzazi wa kulea atahakikisha kwamba mlezi mbadala yeyote anafahamu na anakubali kufuata kanuni zote kuhusu usimamizi na nidhamu.

305 Mzazi wa kulea hatamruhusu mtu mwingine yeyote anayemtunza au kumwangalia mtoto wake wa kulea akiuke kifungu chochote cha kanuni hizi za leseni.

306 Wazazi wa kulea watachukua hatua zinazofaa za kuwalinda watoto wa kulea kutokana na hatari.

Mazingira ya Nyumba, Jamii, na Shughuli za Familia

307 Wazazi wa kulea watoe uzoefu wenye kujenga, na chanya wa maisha ya kifamilia kwa watoto wa kulea.

308 Vifaa na nyenzo zinazofaa kwa umri wa watoto wa kulea vitapatikana kwa ajili ya kucheza kwa kujishughulisha viungo na kwa utulivu.

309 Wazazi wa kulea watapanga mawasiliano ya jamii na kuhimiza urafiki kati ya watoto wa kulea na watoto wengine katika jamii.

310 Wazazi wa kulea watatoa fursa za burudani na shughuli za jamii.

311 Wazazi wa kulea watahakikisha kwamba watoto wa kulea wanahudhuria shule kulingana na sheria za jimbo na mpango wa kulea wa mtoto anayetunzwa.

312 Wazazi wa kulea watahakikisha kwamba majukumu katika kaya au kazi za nyumbani zinafaa kwa umri, kiwango cha ukuaji, na uwezo wa mtoto wa kulea, na haziathiri shule, kulala, kusoma au wakati 8 mzuri wa burudani.

313 Wazazi wa kulea hawatahitaji mtoto atumie pesa alizojipatia kulipia chumba na bweni isipokuwa ikiwa imeidhinishwa na mtunzaji wa mtoto kama sehemu ya mpango wa kulea wa mtoto anayetunzwa.

314 Wazazi wa kulea watawapatia watoto mavazi yanayofaa.

Usiri na Faragha

315 Wazazi wa kulea watachukulia taarifa zote za kibinafsi zinazohusu watoto wa kulea na familia zao kama siri.

316 Wazazi wa kulea hawataidhinisha kuchapishwa kwa jina au picha ya mtoto wa kulea kwa njia inayomtambulisha mtoto kama mtoto wa kulea bila ruhusa kwa maandishi ya mtunzaji wa mtoto.

317 Wazazi wa kulea wataruhusu watoto wa kulea wawasiliane kwa barua na kwa simu kulingana na mpango wa kulea wa mtoto anayetunzwa.

318 Wazazi wa kulea watapanga mazingira ya faragha inavyofaa kwa kushauriana na mawakili na wafanyakazi wa kijamii.

319 Wazazi wa kulea wataheshimu faragha ya mtoto.

Mahusiano na Familia ya Mtoto

320 Wazazi wa kulea wataunga mkono juhudi za kuanzisha na kudumisha mahusiano baina ya watoto wa kulea na familia zao, kama ilivyoainishwa katika mpango wa kulea.

321 Wazazi wa kulea hawatamzuia mtoto wa kulea asitembelewe na mzazi au mlezi kama ilivyoainishwa na hatua ya mahakama au mpango wa kulea.

322 Wazazi wa kulea watashirikiana na shirika la kuwaweka watoto katika kupanga malezi na kutekeleza mpango wa kulea.

Nidhamu

323 Nidhamu itakuwa inayofaa na yenye mafunzo. Marekebisho lazima yafanywe kwa haki, busara, na bila kubadilika, na wakati wowote inapowezekana lazima yahusiane kimantiki na tabia inayohitaji kubadilishwa.

324 Mzazi wa kulea hatamwadhibu mtoto wa kulea kwa mbinu yoyote ya kikatili, ya kudhalilisha au isiyo ya lazima, ikiwemo, bali sio tu:

324.1 Kuchapa, kupiga makofi, kupiga, kutetemesha, au vinginevyo kuumiza mtoto kimwili;

324.2 Kumtaka au kumlazimisha mtoto akae mkao usio mfariji, kama vile kuchuchumaa au kuinama, au kumlazimisha au kumshurutisha mtoto kurudia vitendo vya kimwili pale vinapotumika kama njia ya kuadhibu;

324.3 Kufungiwa kwenye kabati au chumba kilichofungwa;

324.4 Kunyimwa chakula muhimu, maji, mapumziko, au fursa ya kwenda chooni au kuoga;

324.5 Kunyimwa haki za kutembelewa au mawasiliano na familia, mfanyakazi wa kijamii, au wakili kama njia ya kuadhibu;

324.6 Kuzuia hisia kupita kiasi au msisimko;

324.7 Kizuizi cha kemikali, mitambo, au kimwili isipokuwa ilivyoidhinishwa katika Kanuni ya 326.

324.8 Kitendo chochote kinachofafanuliwa kama unyanyasaji au kupuuzwa na Sheria za Vermont Zilizotambuliwa, Kifungu cha 33, Sura ya 49.

325 Wazazi wa kulea hawatakiwi kujihusisha na vitendo vyovyote ambavyo vina athari ya kumdhalilisha mtoto wa kulea, au ambayo inaweza kuzuia mtoto huyo kujithamini.

326 Mzazi wa kulea hapaswi kumzuia kimwili mtoto wa kulea isipokuwa pale ambapo tabia ya mtoto inatishia kumdhuru mtoto mwenyewe au watu wengine au kuharibu sana mali, au pale ambapo kizuizi hicho ni kwa mujibu wa mpango wa matibabu uliowekwa.

326.1 Kiasi cha nguvu kinachotumika katika kumzuia na muda wa zuio lazima kiwe kiwango kidogo zaidi sawa na kupunguza hatari kwa kiwango kinachoweza kudhibitiwa na njia zisizo na vizuizi.

326.2 Wazazi wa kulea watatoa taarifa kwa mtunzaji wa mtoto visa vyote vya kumzuia mtoto wa kulea.

326.3 Wazazi wa kulea wataweka kumbukumbu ya maandishi ya visa vyovyote vya kumzuia mtoto wa kulea kimwili.

327 Wazazi wa kulea hawapaswi kumtenga mtoto wa kulea kuingia kwenye makao isipokuwa ikiwa ni sehemu ya mpango ulioidhinishwa wa kulea.

328 Wazazi wa kulea hawatamwadhibu mtoto kwa sababu ya kukojoa kitandani au kwa sababu ya jinsi ya kutumia choo.

Matunzo Kiafya

329 Wazazi wa kulea watashirikiana na mlezi katika kupata huduma ya kawaida na ya dharura ya matibabu na afya ya akili kwa watoto wanaolelewa, pamoja na uchunguzi wa kawaida wa matibabu na meno, na chanjo.

330 Wazazi wa kulea wataangalia ikiwa watoto wana dalili za maradhi, ugonjwa, au mabadiliko ya tabia na watayashughulikia na kumtunza mtoto anayeugua, aliyepata ajali, au jeraha.

331 Vifaa vya huduma ya kwanza vinapaswa kuwepo kwa ajili ya kutibu majeraha madogo.

332 Wazazi wa kulea hawatamnyima mtoto wa kulea dawa au matibabu au kubadilisha dozi zilizoagizwa bila idhini ya tabibu.

333 Wazazi wa kulea hawatampatia mtoto wa kulea dawa yoyote ambayo mtoto huyo hajaagiziwa.

334 Wazazi wa kulea hawatampa mtoto wa kulea vinywaji vyenye kileo au dawa yoyote ya kulevya.

Chakula na Lishe

335 Wazazi wa kulea watahakikisha kwamba mtoto wa kulea

anapatiwa milo angalau mitatu au chakula kama hicho kwa siku, kinachopatikana kwa masaa ya kawaida.

336 Wazazi wa kulea watatoa lishe bora inayotosha ili kukidhi mahitaji ya lishe ya kila mtoto wa kulea.

337 Familia ya kulea itawajumuisha watoto wa kulea wakati wa chakula cha familia na itawapa chaguo sawa la chakula kama wanafamilia wengine, kwa kuzingatia mahitaji ya lishe na mapendekezo binafsi.

Dini na Urithi Kiutamaduni

338 Wazazi wa kulea wataheshimu imani za kidini na urithi kiutamaduni wa watoto wa kulea, na hawataingilia desturi nzuri ya imani za kidini za mtoto wa kulea.

339 Wazazi wa kulea hawatalazimisha mtoto anayelelewa ashiriki katika shughuli za kidini au hafla za kikabila ikiwa mtoto hataki.

Kutoa Taarifa na Tahadhari

340 Mzazi wa kulea atatoa taarifa kwa Ofisi ya Wilaya ya eneo hilo kuhusu hali zozote zinazoonyesha kuwa mtoto anayelelewa amenyanyaswa kama inavyofafanuliwa na 33 VSA au amekuwa mwathiriwa wa kushambuliwa kimwili au unyanyasaji mwingine wa kimwili au wa kingono.

341 Wazazi wa kulea watamjulisha mtunzaji wa mtoto:

341.1 Mara tu itakapobainika kuwa mtoto wa kulea amekimbia au amepotea;

341.2 Kabla ya kupanga mipango ya utunzaji wa mtoto na watu wengine kwa kipindi chochote zaidi ya saa arobaini na nane, au kwa mpango wowote wa kutokuwepo kwa mtoto katika makao ya kulea zaidi ya saa arobaini na nane;

341.3 Mwanafamilia yeyote akiwa na ugonjwa unaoweza kusababisha tishio kubwa kwa afya ya mtoto wa kulea;

341.4 Mtoto wa kulea akiwa na ugonjwa mbaya au jeraha.

342 Mmiliki wa leseni ataijulisha mamlaka ya leseni ya jimbo wakati yoyote kati ya yafuatayo yanapotokea au yanatarajiwa:

342.1 Familia ya kulea ikihamia katika majengo tofauti;

342.2 Kukiwa na mabadiliko, yasiyohusu watoto wa kulea, katika familia;

342.3 Kukiwa na mabadiliko nyumbani, yanayoathiri kufuata kanuni hizi;

342.4 Familia inapanga kutumia mipangilio ya kulala mbali na ile iliyoidhinishwa hapo awali;

342.5 Kuna ugonjwa mbaya wa kimwili au kiakili au mwana kaya yeyote ameumia, ambapo inaweza kuathiri uwezo wa familia ya kulea kutoa matunzo kwa watoto;

342.6 Familia inakusudia kutoa matunzo kwa watoto au watu wazima wanaotegemewa kupitia mpango au shirika zaidi ya moja.

MAZINGIRA YA NJE

Usalama na Matengenezo ya Jumla

401 Mzazi wa kulea atatunza nyumba, viwanja na vifaa vya nje na atahakikisha kwamba hakuna dhara au hatari yoyote isiyofaa.

402 Makao ya kulea yatakuwa na joto na hewa ya kutosha.

403 Wazazi wa kulea watahakikisha kuwa watoto walio chini ya ulinzi wa Idara hawaathiriwi na moshi wa sigara katika nyumba ya mzazi au gari.

404 Makao ya kulea yatakuwa na huduma ya simu.

405 Jiko katika nyumba ya kulea litakuwa na sinki na maji ya bomba na vifaa vingine vyote muhimu vya utayarishaji na uhifadhi salama wa chakula.

406 Nyumba ya malezi itakuwa na angalau bafu moja ya ndani

na choo cha kuflashi, beseni yenye maji ya bomba, na bafu moja au bafu yenye maji ya moto na baridi.

407 Silaha ya moto yoyote itawekwa katika hifadhi iliyofungwa na ambapo risasi zitahifadhiwa tofauti katika nafasi iliyofungwa, au haitafanya kazi kwa kufunga sehemu muhimu za silaha au kuondolewa na kufungwa kwa sehemu hizo.

408 Wazazi wa kulea wataweka dawa na vifaa vyenye hatari mbali na watoto.

409 Nambari za simu za dharura, pamoja na zimamoto, polisi, daktari, udhibiti sumu, shirika la afya na gari la wagonjwa, zitawekwa wazi karibu na simu.

410 Wazazi wa kulea watawazuia watoto wa kulea wasifikiwe na wanyama hatari.

411 Wazazi wa kulea watahifadhi vifaa vyote vinavyoendeshwa na nguvu vinavyotumiwa na watoto wa kulea katika hali salama, na kuhakikisha kwamba vifaa vyote vya usalama viko mahali pao na vinafanya kazi.

411.1 Wazazi wa kulea watatoa mwelekeo unaofaa na usimamizi wakati mtoto anayelelewa anatumia vifaa kama hivyo.

Usalama kwa Moto

412 Nyumba husika haitakuwa na hatari ambayo ni hatari ya wazi ya moto, kama vile nyaya za umeme zenye makosa, soketi zilizojaa zaidi za umeme au mkusanyiko wa karatasi, rangi au vifaa vingine vya kuwaka vinavyohifadhiwa kwenye nyumba hiyo.

413 Wazazi wa kulea watakuwa na mpango wa uokoaji utakaotumika wakati wa moto na watahakikisha kwamba, watoto wa kulea wanauelewa mpango huo kulingana na

uwezo wao wa kuelewa. Mpango unapaswa kujumuisha:

413.1 Maelezo ya njia mbili au zaidi za kutoka kwa kila ngazi ya sakafu inayotumiwa kulala na watoto wa kulea;

413.2 Mahali pa watu wote kukusanyika nje ya nyumba; na,

413.3 Njia ya kuhamisha watoto ambao wanahitaji msaada.

414 Wazazi wa kulea watatoa idadi ya kutosha ya vitambuzi moshi, ambavyo vimewekwa vizuri, vinapatikana na vinafanya kazi. Kutakuwa na angalau kitambuzi kimoja kama hicho kwenye sakafu ya chini na moja kwenye kila sakafu ambayo hutumiwa kama mahali pa kuishi.

415 Wazazi wa kulea wataweka kifaa cha kuzima moto cha aina ya ABC katika eneo la kupikia la makao.

416 Kutakuwa na angalau njia mbili za kutokea zinazoweza kupatikana kutoka kila ngazi ya sakafu inayotumiwa na watoto wa kulea kulala.

Sera Kuhusu Vifaa vya Kutambua Moshi na Vifaa vya kutambua Kaboni Monoksaidi

Sera # 225 inabainisha zaidi kwamba lazima kuwe na kitambuzi moshi na kaboni monoksaidi kwenye kila sakafu na maeneo yaliyo karibu sana na vyumba vyote vya kulala.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Kitengo cha Leseni ya Makazi.

Sera Kuhusu Njia ya Pili ya Kutoka katika Vyumba vya Kulala

Sera # 225 inabainisha zaidi kuwa kila chumba cha kulala kinachotumiwa na mtoto wa kulea lazima kiwe na angalau njia mbili za kutoka.

Ya msingi itakuwa mlango wa chumba cha kulala cha kuingia ndani ya nyumba. Ya pili inaweza kuwa moja kati ya zifuatazo:

- Mlango wa pili kutoka chumba cha kulala kuelekea moja kwa moja nje ya nyumba;
- Mlango wa pili kutoka chumba cha kulala kuelekea kwenye kibaraza cha ghorofani; au
- Dirisha la nje (kubwa vya kutosha kutumika kama njia ya uokoaji au kutoroka) ambayo sio zaidi ya futi 20 kutoka ardhini au inafungukia kwa kutua nje, paa, kibaraza cha ghorofani, au sitaha.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Kitengo cha Leseni ya Makazi.

Vyumba vya kulala

417 Kila mtoto wa kulea atapewa kitanda chake au kitenga.

418 Hakuna mtoto wa kulea mwenye zaidi ya miaka miwili atakayelala katika chumba kimoja na mtu mzima.

419 Hakuna mtoto mwenye umri wa zaidi ya miaka mitano atakayelala katika chumba kimoja na mtoto wa jinsia tofauti wakati mtoto yeyote ni mtoto wa kulea.

420 Hakutakuwa na watoto zaidi ya wanne walioteuliwa kulala kwenye chumba cha kulala wakati yeyote kati yao ni mtoto wa

kulea.

421 Hakuna sebule, eneo la kulia chakula au eneo lingine la nyumba, ambalo kwa kawaida si chumba cha kulala, linaloweza kutumiwa kwa sababu hiyo na mwana kaya yeyote mara kwa mara.

422 Chumba cha kulala kinachotumiwa na mtoto wa kulea kitakuwa na ukubwa wa kutosha ili kuwe na kitanda na nafasi ya kuvaa, shughuli za utulivu na kuweka mali za wakazi wa chumba hicho.

423 Vyumba vyote vya kulala na bafu zinazotumiwa na watoto wa kulea zitakuwa na milango ambayo inaweza kufungwa na ambayo inaweza kufunguliwa kwa urahisi kutokea ndani.

424 Chumba cha kulala kinachotumiwa na mtoto wa kulea kitakuwa na angalau dirisha moja, ambalo linaweza kufunguliwa kuelekea nje.

425 Maeneo ya chumba cha kulala yatafikiwa kupitia mahali pa kuingilia tofauti na bafuni.

426 Angalau bafu moja itafikiwa kwa njia ya kuingia isiyokuwa chumba cha kulala.

427 Chumba cha kulala, ambacho kinapatikana tu kupitia chumba kingine cha kulala, kinaweza kutumiwa tu wakati wenyeji wa vyumba viwili vya kulala wangeweza kulala katika chumba cha kulala chini ya masharti ya kanuni hizi.

428 Kila mtoto wa kulea atakuwa na godoro safi na atapewa matandiko safi yanayofaa kulingana na msimu.

429 Vitanda vyote vilivyotengwa kutumiwa na watoto wa kulea vitakuwa na nafasi ya kutosha kichwani ili kumruhusu mtoto akae vizuri kitandani.

430 Wazazi wa kulea watampa kila mtoto wa kulea kabati ya nguo au nafasi nyingine ya kutosha ya kuhifadhia na nafasi ya kutundika nguo karibu na chumba cha kulala cha mtoto.

Usafirishaji

431 Wazazi wa kulea watakuwa na usafiri wa kawaida kwa ajili ya watoto wa kulea.

432 Wazazi wa kulea watatunza magari yanayotumika kusafirisha watoto wa kulea katika hali salama na watahakikisha kuwa magari hayo yamesajiliwa vizuri, kukaguliwa na yana bima.

433 Watoto wa kulea watasafirishwa tu na mtu mwenye leseni halali ya udereva.Wazazi wa kulea watahakikisha kwamba mtoto yeyote wa kulea mwenye uzito wa chini ya pauni arobaini au mtoto yeyote wa kulea mwenye umri wa chini ya miaka mitano amewekwa vizuri katika mfumo wa kuzuia watoto wachanga au mtoto abiria wakati wa kusafirishwa kwa gari la wazazi wa kulea. Wazazi wa kulea watahakikisha kwamba watoto wengine wote wa kulea wamefungwa vizuri mikanda ya kiti wakati wanasafirishwa kwa gari la wazazi wa kulea.

ILANI MUHIMU:
Sheria ya Vermont Inaboresha Usalama wa Abiria Mtoto

Kuanzia Januari 1, 2004, sheria ya Vermont inasema kwamba hakuna mtu atakayeendesha gari, isipokuwa basi ya aina 1 ya shule, katika jimbo hili kwenye barabara kuu ya umma isipokuwa kila mtu aliye chini ya umri wa miaka 16 aliyezuiliwa vizuri katika mfumo wa kuzuia abiria watoto uliowekwa na serikali kama ilivyoainishwa katika 49 CFR §571.213 (1993) au mkanda wa usalama ulioidhinishwa na serikali, kama ifuatavyo:

- Watoto wote wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, na watoto wote wenye uzito wa chini ya pauni 20, bila kujali umri, watazuiliwa kwa kuangalia nyuma, wakiwa salama katika mfumo wa kuzuia abiria mtoto uliokubaliwa na serikali, ambao hautawekwa mbele ya mfumo wa begi la hewa inayotumika;
- Mtoto mwenye uzito wa zaidi ya pauni 20, na ambaye ana umri wa mwaka mmoja au zaidi na chini ya umri wa miaka nane, atazuiliwa katika mfumo wa kuzuia abiria mtoto (Hii inamaanisha viti vya usalama vya watoto vinavyorekebishika, vyote na nyongeza za viti); na
- Mtoto mwenye umri wa miaka nane hadi 15 atazuiliwa katika mfumo wa mkanda wa usalama au mfumo wa kuzuia abiria mtoto.

Kwa taarifa zaidi, wasiliana na Mpango wa Usalama ya Barabara Kuu kupitia namba 1-888-868-7328 au tembelea tovuti yao *http:www.dps.state.vt.us/ghsp/*.

FASILI

Mwombaji

Mtu ambaye ameleta ombi rasmi, kwa maandishi la leseni ya makao ya kulea.

Mlezi
Mtu ambaye anatoa matunzo na usimamizi kwa mtoto wa kulea.

Mpango wa Kulea
Mpango wa utoaji wa huduma kwa mtoto wa kulea, ulioandaliwa na shirika linalowajibika kutoa huduma hizo.

Kamishna
Kamishna wa Idara ya Watoto na Familia.

Mtunzaji
Mtu au shirika (kama vile Idara ya Watoto na Familia) aliye na haki ya ulezi wa kisheria wa mtoto.

Kukataa
Uamuzi rasmi wa mamlaka ya leseni ya serikali wa kutompatia mwombaji leseni ya makao ya kulea.

Mtu mzima Anayetegemea
Mtu mzima ambaye anahitaji, na anapata, utunzaji binafsi na / au anasimamiwa.

Huduma ya Kulea
Utoaji wa utunzaji wa masaa 24 kwa siku katika nyumba ya familia kwa mtoto ambaye si mtoto wa kibaolojia au aliyechukuliwa na mtoaji.

Mtoto wa Kulea
Mtoto anayepokea huduma ya kulea.

Makao ya Kulea
Majengo ambayo huduma ya malezi hutolewa na wana kaya wanaishi.

Mzazi wa kulea
Mtu aliye na leseni ya kutoa malezi; mtu anayetakiwa na sheria ya jimbo kuwa na leseni hiyo.

Mwana kaya
Mtu yeyote, iwe ni mwanafamilia au mtu mwingine, anayeishi na kulala mara kwa mara katika makao ya kulea.

Leseni
Idhini kutoka kwa mamlaka ya leseni ya jimbo kwa watu walioteuliwa kutoa malezi ya watoto katika eneo lililotengwa; cheti kinachotoa idhini hiyo.

Mmiliki wa leseni
Mtu ambaye jina lake limeandikwa kwenye leseni.

Kizuizi cha Kimwili
Mzazi wa kulea kumzuia mtoto moja kwa moja kimwili ili mtoto asijiumize yeye mwenyewe, asiumize wengine, au asiharibu mali.

Mlezi wa Msingi
Mtu mzima ambaye humtunza na kumsimamia mtoto wa kulea katika makao ya kulea mara kwa mara.

Kufutwa
Ubatilishaji rasmi, ya leseni na mamlaka ya leseni ya jimbo.

Mamlaka ya Leseni ya Jimbo
Shirika jimboni humo lililo na mamlaka kisheria ya kutoa leseni kwa makao ya kulea.

Kusimamishwa
Kubatilishwa kwa leseni kwa muda na mamlaka ya leseni ya jimbo katika hali ambayo inahatarisha afya, usalama au ustawi wa mtoto wa kulea haraka.

Mbadala wa kanuni
Idhini kwa maandishi ya mamlaka ya leseni ya jimbo kwa mwombaji au mmiliki leseni ili kutimiza mahitaji ya kanuni kwa njia nyingine ambayo siyo iliyopo kwenye kanuni.

Ofisi za Wilaya Divisheni ya Huduma za Familia

Barre: (802) 479-4260

Bennington: (802) 442-8138

Brattleboro: (802) 257-2888

Burlington: (802) 863-7370

Hartford: (802) 295-8840

Middlebury: (802) 388-4660

Morrisville: (802) 888-4576

Newport: (802) 334-6723

Rutland: (802) 786-5817

Springfield: (802) 289-0648

St. Albans: (802) 527-7741

St. Johnsbury: (802) 748-8374

dcf.vermont.gov/fsd

09/20 • 1,000